# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## OFISI YA WAZIRI MKUU-TAMISEMI
### HALMASHAURI YA WILAYA CHATO

**Namba za simu**

Mkuu wa Shule ***0782157318***
Makamu Mkuu wa Shule ***0656412249***
Matron ***0655218897***
***Email:jikomboehighschool@yahoo.com***

SHULE YA SEKONDARI JIKOMBOE,
S.L.P 190,
**CHATO - GEITA**

---

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi………………………………
S.L.P ……………
……………………

**YAH: MAELEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI JIKOMBOE HALMASHAURI YA WILAYA CHATO MKOA WA GEITA MWAKA ……….**

Ninayofuraha kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii mwaka **……** tahasusi ya **HGL/HKL/HGK/HGE.** Nakupongeza na karibu sana Jikomboe.

Muhula wa masomo unaanza tarehe **………..** Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni **………..** Mwisho wa kuripoti ni tarehe **………..**. Ukifika shuleni utapokelewa na Makamu Mkuu wa Shule na kusajiliwa katika daftari maalumu la kusajilia wanafunzi (Student Admission Register Book)

**MAHALI SHULE ILIPO**

Shule ya Sekondari Jikomboe, ambayo ni ya wasichana pekee, ipo katika Wilaya ya Chato katika Mkoa wa Geita Kata ya Muungano kitongoji cha Mifugo. Kuna umbali wa kilometa 3 kutoka stendi kuu ya mabasi mpaka shule ilipo.

**NAMNA YA KUSAFIRI KUFIKA SHULE YA SEKONDARI JIKOMBOE**

1. Kwa wanaopitia au kuanzia safari zao Mwanza wanapanda mabasi yaendayo Bukoba au yanayoishia Muganza na kuteremka Chato.
2. Kwa wanaotoka Dar es Salaam Morogoro, Dodoma au Singida wanaweza kupanda mabasi yaendayo Mwanza kisha apande mabasi ya Mwanza-Chato au anaweza kupitia Mwanza na kupanda mabasi yaendayo Bukoba na kuteremka Chato.
3. Kwa wanaotoka Karagwe kupitia Bukoba, watapanda mabasi yaendayo Mwanza na watashukia Chato.
4. Kwa wanaotoka Kigoma, watapanda mabasi yaendayo Mwanza kupitia Runzewe wakifika Bwanga watashuka na kupanda magari yaendayo Chato- Muganza
5. Kwa wanaotoka Ngara kupitia Biharamulo, wakifika Biharamulo watapanda magari madogo yaendayo Chato.

   **NB:** Wote hawa wakifika Chato wateremka stendi kuu ya mabasi Kahumo (Itale) Wakiulizia

mtu yeyote atawaonyesha shule ilipo na usafiri unaotumika kutoka standi mpaka shule ni boda boda au bajaji.

## 2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### 2.1 Sare za Shule

a. Sketi mbili (2) rangi ya kijivu iliyoiva (Istimu namba 1) zinapatikana shuleni
b. Hijab nyeupe (kijuba) ifanane na sare ya shule (kwa waislamu)
c. Sare za michezo
   - Uje na raba nyeupe na soksi/stockings za bluu
   - Bukta ndefu na t-shirt rangi ya bluu (t-shirt ya Taifa stars)
d. Uje na viatu vya shule vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino.
e. Soksi jozi mbili nyeupe ndefu (Stockings)
f. Sweta 1 rangi ya kijivu iliyoiva yenye nembo ya shule (Inapatikana shuleni)
g. Nguo za kushindia (Shamba dress)
   - Gauni mbili (2) rangi ya blue bahari kitamba cha (Istimu namba 1) zinapatikana shuleni
   - Tshirt 1 rangi ya dark blue yenye nembo ya shule (inapatikana shuleni)
h. Tai 2 rangi ya kijivu iliyo iva kitamba cha sketi
i. Tracksut- (suruali na jaketi lake rangi ya dark blue) Sare ya kuvaa wakati wa masomo ya usiku.
j. Shati mbili (2) nyeupe mikono mirefu (kitambaa cha haluwa)

**NB. Wazazi ambao upatikanaji wa sare za shule utakuwa mgumu kupatikana wawasiliane na uongozi wa shule kwa msaada zaidi.**

### 2.2 Michango ya shule

a. Michango yote ilipwe kwenye Akaunti ya shule **JIKOMBOE HIGH SCHOOL RECCURENT ACCOUNT: Ac. No. 32701200082 NMB.** (Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip)

**Mchanganuo wa michango;**

i. Shilingi 65,000/= kwa ajili ya uendeshaji
ii. Shilingi 5,000/= kwa ajili ya tahadhari
iii. Shilingi 5,000/= kwa ajili ya nembo
iv. Shilingi 5,000/= kwa ajili ya kitambulisho

**Jumla ya michango yote ni 80,000/=**

### 2.3 Bima ya afya;

**Jukumu la matibabu ni la mzazi, hivyo mzazi, mlezi anashauriwa kumlipia mtoto wake bima ya afya ya taifa (NHIF) ambapo shule itawaunganisha na ofisi za NHIF mkoa wa Geita kupata bima hizo, kila mwanafunzi ni lazima aje na bima ya afya ya NHIF. Kwa wale wasiokua nazo waje na shilingi 50,400/= ili wapatiwe bima hizo na ofisi za bima (NHIF) mkoa wa Geita malipo hayo ya bima ni kwa mwaka.**

b. **Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni:-**

- HGE na HGL waje na Fyekeo, Mopa, soft broom na chelewa mbili (2).
- HGK na HKL waje na hard broom (brash), jembe na mpini wake, brashi ndogo za chooni na Squizer
- Godoro futi 2 ½
- Chandarua pembe nne rangi nyeupe
- Ndoo mbili, moja yenye ujazo wa lita 20 na nyingine lita 10
- Chombo chenye ujazo wa lita 5 cha kuhifadhi maji ya kunywa
- Bakuli, sahani, kikombe, na kijiko kwa ajili ya uji na chakula
- Kalamu za kutosha na vifaa vya kuchorea kwa mchepuo wa HGL,HGK na HGE
- Flatfile kwa ajili ya kutunza kumbukumbu zako.
- Counterbooks 11 za 4Quire au 3Quire
- Ream 1 A4 kwa kila mhula wa masomo
- Oxford Advanced Learners Dictionary kwa matumizi yako na Kamusi ya Kiswahili
- Scientific Calculator kwa wale wa mchepuo wa HGL, HGK na HGE
- Hati maalumu ya vipimo vya daktari kuthibitisha hali ya afya yako (fomu imeambatishwa )

**NB: Mahitaji mengine yanapatikana duka la shule, daftari, kalamu, file, na vifaa vingine.**

## 2.4 MAVAZI, NGUO NA MAHITAJI BINAFSI

- Jozi moja ya kanga
- Taulo
- Kanda mbili za kuogea
- Underskirts mbili au zaidi na nguo za ndani zisizopungua 12 na pads bunda 5
- Shuka mbili za pink na shuka 2 za blue pamoja na blanketi moja
- Nguo za kulalia
- Sabuni za kuogea na kufulia

## 3. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

1. *Wizi.*
2. *Uasherati na ushoga.*
3. *Ubakaji.*
4. *Ulevi matumizi ya madawa ya kulevya kama vile* ***bangi****,* ***cocane****,* ***milungi****,* ***kubeli*** *nk.*
5. *Kupigana au kupiga.*
6. *Kuharibu makusudi mali ya umma.*
7. *Kudharau bendera ya Taifa.*
8. *Kuolewa/kuwekwa kimada.*
9. *Kupata mimba/kutoa mimba.*
10. *Kugoma,kuchochea, kugoma au kuivuruga amani na usalama wa shule au watu.*
11. *Kugoma adhabu kwa makusudi.*
12. *Mwanafunzi kuwa na* ***simu ya mkononi.***
13. *Udanganyifu wa aina yoyote katika mitihani.*
14. *Kutotii serikali iliyopo madarakani.*
15. *Kuwa nje ya mazingira ya shule bila kuwa na sare ya shule na ruhusa ya Mkuu wa shule au Mwalimu wa zamu.*
16. *Ni marufuku kutumia vifaa vya umeme kama vile* ***JAGI****, au* ***HEATER*** *ya kuchemshia maji.*
17. *Ni marufuku kutumia vipodozi vya aina yoyote ile.*
18. *Marufuku kununua au kuingiza vyakula vya aina yoyote shuleni bila ruhusa ya mwalimu wa chakula.*

***MUHIMU:***

- ***Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;***
- ***Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;***
- ***Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalumu kutoka kwa mkuu wa shule (msiba au ugonjwa).***
- ***Mwanafunzi hapaswi kuja na nguo yoyote ya nyumbani tofauti na zile zilizoainishwa kwenye fomu hii.***

**4. Viambatanisho na Fomu Muhimu**

a) Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya serikali.

b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai.

c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

d) Picha nne (4) za wazazi na Ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.

Unatakiwa kutii sheria, taratibu na kanuni za shule muda wote uwapo shuleni. Kutojua sheria za shule haitakuwa kinga ya kutokuchukuliwa hatua.

Kwa kipindi chote utakachokuwa mwanafunzi wa shule hii utakuwa unawakilisha shule na popote pale utakapokuwa. Hivyo basi utovu wa nidhamu utakaofanya bila ya kujali mahali au wakati, uongozi wa shule utachukua hatua za kinidhamu zinazo stahili dhidi yako.

………………………………

**MECKTILDA G. HERMAN**

**MKUU WA SHULE**

THE HEADMISTRESS
JIKOMBOE SECONDARY SCHOOL
P.O.Box 190 CHATO

***Mawasiliano 0782157318***

*"KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI JIKOMBOE"*

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## OFISI YA WAZIRI MKUU-TAMISEMI
### HALMASHAURI YA WILAYA CHATO

**Namba za simu**

Mkuu wa shule ***0782157318***
Makamu Mkuu wa Shule ***0656412249***
Matron ***0655218897***
***Email:jikomboehighschool @yahoo.com***

SHULE YA SEKONDARI JIKOMBOE,
S.L.P 190,
**CHATO - GEITA**

---

**MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI**

Sehemu hii ijazwe na mwanafunzi:

1. Jina kamili la mwanafunzi:……………………………………………………………………
2. (a) Tarehe ya kuzaliwa:…………………………………………………………………………
   (b) Kijiji/Mtaa alipozaliwa…………………………………………………………………………
3. (a)Dini:…………………………………………………………………………………
   (b) Dhehebu:…………………………………………….……………………..
4. (a) Ni raia wa Tanzania? (Jibu NDIYO au HAPANA)…………………………………………
   (b) Kama siyo Mtanzania, taja uraia wako na ulete cheti cha uraia:………………………
5. (a) Darasa ulilomaliza:………………………………………………………………………
   (b) Shule ulikotoka:…………………………………………………………………
6. (a) Jina kamili la Baba/Mama/Mlezi:…………………………………………………
   (b) Anwani ya Mzazi/Mlezi:………………………………………………………………
   (c) Namba ya simu ya Mzazi/Mlezi:……………………………………………………
7. (a) Mahali unapoishi:………………………………………………………………………
   (b) Ni umbali gani kutoka shuleni?.........................................................................................
8. (a) Unaishi na nani? Taja jina lake kamili:……………………………………………
   (b) Una uhusiano gani na huyo uliyemtaja?.........................................................................
   (c) Unaishi katika nyumba ya kupanga? (Jibu NDIYO au HAPANA)……………………………
9. Mzazi/Mlezi anafanya kazi gani?...........................................................................................
10. Je una ndugu Chato? (Jibu NDIYO au HAPANA). Kama ndiyo,
    anaitwa nani?..................................................uhusiano …………………………..……………
    Anaishi wapi…………………………………………………………..…………

Namba yake ya simu……………………………………………..……………….

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU-TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA WILAYA CHATO**

**Namba za simu**

Mkuu wa shule ***0782157318***
Makamu Mkuu wa Shule ***0656412249***
Matron ***0655218897***
***Email:jikomboehighschool @yahoo.com***

SHULE YA SEKONDARI JIKOMBOE,
S.L.P 190,
**CHATO - GEITA**

---

## SHERIA ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya elimu nchini. Kila mwanafunzi anatakiwa kushika na kuheshimu sheria, taratibu na kanuni za shule. Kutojua sheria hakutakuwa kinga ya kutochukuliwa hatua. Sheria hizo ni kama ifuatavyo:-

1. **HESHIMA**
   Kila mwanaufnzi anapaswa kuheshimu viongozi, Wazazi, Walimu na wanafunzi wenzake.

2. **UTORO**
   Utoro wa aina yoyote hauruhusiwi hapa shuleni. Mwanafunzi anatakiwa kuwepo shuleni toka siku ya kufungua shule mpaka siku ya kufunga shule na anatakiwa kuhudhuria vipindi vyote darasani siku zote awapo shuleni.

3. **MAANDALIO**
   Kila mwanafunzi anatakiwa kuhudhiria maandalio (night/morning preparation time) kushindwa kufanya hivyo ni kosa na atachukuliwa hatua.

4. **KUWAHI**
   Kila mwanafunzi anatakiwa kuwahi parade na katika shughuli mbalimbali za shule na anatakiwa kutii kengere.

5. **USAFI**
   Kila mwanafunzi anatakiwa kutunza usafi wa mwili, bweni na mazingira ya shule.

6. **SARE YA SHULE**
   Kila mwanafunzi anatakiwa kuvaa sare sahihi ya shule kulingana na ratiba ya shule inavyomtaka.

7. **RATIBA YA SHULE**
   Kila mwanafunzi anapaswa kuzingatia ratiba ya shule.

8. **KUWA NJE YA SHULE**
   Mwanafunzi yeyote yule hatakiwi kwenda nje ya mazingira ya shule bila ruhusa ya mwalimu wa

zamu/mlezi au mkuu wa shule. Endapo atapewa ruhusa anatakiwa avae sare ya shule.

**9. MAWASILIANO**

Kiingereza ndiyo lugha ya mawasiliano hapa shuleni isipokuwa wakati wa kipindi cha Kiswahili. Mwanafunzi anatakiwa kuongea Kiingereza muda wote awapo bwenini, darasani au katika shughuli za nje.

**10. SIMU YA MKONONI**

Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na **simu ya mkononi** ukibainika adhabu yake ni kufukuzwa shule.

11. Wizi, uasherati, ushoga, ubakaji, ulevi na ugomvi ni marufuku kwa mwanafunzi yeyote.

12. Kubeba mimba ni **marufuku** ukibainika adhabu yake ni kufukuzwa shule.

**13. SIKU ZA KUTEMBELEA WANAFUNZI**

Mzazi/Mlezi ndiye anayeruhisiwa kumtembelea mwanafunzi kila Jumamosi ya mwisho wa mwezi wa pili na mwezi wa nane kila mwaka wa masomo.

14. Mawasiliano yote yanatakiwa kufanyika kupitia kwa Mkuu wa shule na si vinginevyo.

15. Mwanafunzi yeyote atakaye toka nje ya shule kwenda kuabudu au kwa shughuli nyingine yoyote ile, haruhusiwi kununua bidhaa yoyote ile bila idhini ya mwalimu wa zamu/mlezi.

***ANGALIZO;***

- **Mwanafunzi atakayebainika kuruka, kutoboa au kuvunja fensi/uzio wa shule atatozwa faini ya kuleta tofali 200 za block. Hivyo mzazi hakikisha mwanao anatulia shuleni na kufuata taratibu za kutoka nje ya shule.**

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## OFISI YA WAZIRI MKUU-TAMISEMI
### HALMASHAURI YA WILAYA CHATO

**Namba za simu**

Mkuu wa shule ***0782157318***
Makamu Mkuu wa Shule ***0656412249***
Matron ***0655218897***
***Email:jikomboehighschool@yahoo.com***

SHULE YA SEKONDARI JIKOMBOE,
S.L.P 190,
**CHATO - GEITA**

---

**FOMU YA KUKUBALI**

**PICHA YA MWANAFUNZI**

**A: MWANAFUNZI**

Mimi ........................................................................ambaye ni mwanafunzi niliyechaguliwa kujiunga na shule ya Sekondari Jikomboe, nakubali kuchukua nafasi niliyopewa ya kidato cha ……………

Katika Shule ya Sekondari Jikomboe. Naahidi kuwa, nitatii na kufuata sheria, taratibu na kanuni zote za shule.

……………………………  …………………………
Sahihi ya Mwanafunzi  Tarehe

---

**PICHA YA MZAZI/MLEZI**

**B: MZAZI/MLEZI**

Mimi………………………………………………….Mzazi/Mlezi wa……………………………… Nimeyasoma masharti yote ya mwanangu kujiunga na Shule ya Sekondari Jikomboe.

Ninakubali na kuahidi kuwa mwanangu atafuata na kutii masharti yote ya shule. Aidha naahidi nitawajibika kwa kumlipia ada ya shule mwanangu pamoja na michango mbalimbali ya shule na nitakuwa tayari kushirikiana na shule pindi nitakapotakiwa kufanya hivyo.

……………………………                                                   ……………………………

Sahihi ya Mzazi/Mlezi                                                           Tarehe

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## OFISI YA WAZIRI MKUU-TAMISEMI
### HALMASHAURI YA WILAYA CHATO

**Namba za simu**

Mkuu wa shule ***0782157318***
Makamu Mkuu wa Shule ***0656412249***
Matron ***0655218897***
***Email:jikomboehighschool@yahoo.com***

SHULE YA SEKONDARI JIKOMBOE,
S.L.P 190,
**CHATO - GEITA**

---

**KIAMBATANISHO B**
**MEDICAL EXAMINATION FORM**

(To be completed by a medical office)
Student name …………………………………………………………………………………
Age ……………………………………………………………………………………………
Blood examination: Haemaglobin ………………………………………………………………….
Any abnormalities Notes …………………………………………………………………………
Stool examination ……………………………………………………………………………..
Urinalysis ………………………………………………………………………………………
T.B Test (If negative Immunizations given) ………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………….
……………………………………………………………………………………………………..
Eyes …………………………………………………………………………………………….
Chest ……………………………………………………………………………………………
Any chronic complaints not noted above e.g.
Asthma ………………………………………………………………………………………….
Headache ……………………………………………………………………………………..
Skin disease etc ………………………………………………………………………………….
…………………………………………………………………………………………………
Also anything else that the school staff should know
About …………………………………………………………………………………………….
……………………………………………………………………………………………………….
Any treatment given or recommended …………………………………………………………………
In case of Bilharzias it's recommended that student should attend the Bilharzias clinic before they come to school ……………………………………………………………………………………………..
I certify that I have examined the above student and recommended that she/he fit unfit to pursue Secondary education.

Signature of examiner………………..

Designation ………………………….
Official stamp ……………………
Date ……………………………

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## OFISI YA WAZIRI MKUU-TAMISEMI
### HALMASHAURI YA WILAYA CHATO

**Namba za simu**

Mkuu wa shule ***0782157318***
Makamu Mkuu wa Shule ***0656412249***
Matron ***0655218897***
***Email:jikomboehighschool@yahoo.com***

SHULE YA SEKONDARI JIKOMBOE,
S.L.P 190,
**CHATO - GEITA**

## NAMNA YA USHONAJI WA SARE NA JINSI ZINAVYOTAKIWA KUWA






TANZANIA



# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## OFISI YA WAZIRI MKUU-TAMISEMI
### HALMASHAURI YA WILAYA CHATO

**Namba za simu**

Mkuu wa shule ***0782157318***
Makamu Mkuu wa Shule ***0656412249***
Matron ***0655218897***
***Email:jikomboehighschool@yahoo.com***

SHULE YA SEKONDARI JIKOMBOE,
S.L.P 190,
**CHATO - GEITA**

**OROADHA YA BAADHI YA VITABU AMBAVYO MWANAFUNZI ANAPASWA KUJANAVYO**

| TAHASUSI | VITABU |
|---|---|
| **HKL** | *Advanced Learner's History Forms 5&6* (By TIE)<br>*Basic Facts About The World History Forms 5&6* (By Shibitali) |
| | *Nadharia ya Lugha Kidato cha 5&6* (By Masebo) |
| | *Misingi ya Ukalimani na Tafsiri* (By Simiyu Wanjala)<br>*Kiswahili kidato cha 5 & 6 (By TIE)* |
| | *Advanced English Dictionary* |
| | *Advanced Level English,* (By TIE)<br>*Competence in Linguistics (By Mgonja)* |
| | *Academic Communications (By TIE)* |
| **HGK** | *Advanced Learner's History Forms 5&6* (By TIE)<br>*Basic Facts About The World History Forms 5&6* (By Shibitali) |
| | *Advanced English Dictionary* |
| | *Physical Geography* (By TIE) |
| | *Practical Geography* (By TIE) |
| | *Nadharia ya Lugha Kidato cha 5&6* (By Masebo) |
| | *Misingi ya Ukalimani na Tafsiri* (By Simiyu Wanjala)<br>*Kiswahili kidato cha 5 & 6 (By TIE)* |
| | *Academic Communications (By TIE)* |
| **HGL** | *Advanced Learner's History Forms 5&6* (By TIE)<br>*Basic Facts About The World History Forms 5&6* (By Shibitali) |
| | *Advanced English Dictionary* |
| | *Advanced Level English,* (By TIE)<br>*Competence in Linguistics (By Mgonja)* |
| | *Physical Geography* (By TIE) |
| | *Practical Geography* (By TIE) |
| | *Academic Communications (By TIE)* |
| **HGE** | *Advanced Learner's History Forms 5&6* (By TIE)<br>*Basic Facts About The World History Forms 5&6* (By Shibitali) |
| | *Physical Geography* (By TIE) |
| | *Practical Geography* (By TIE) |

| | |
|---|---|
| | *Micro and Macro Economics (By TIE)* |
| | *Academic Communications (By TIE)* |
| | *Basic Applied Mathematics (By TIE)* |